Uinjilisti

(Evangelism)

na

Ellis P. Forsman

Uinjilisti

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Uinjilisti

2 Tim. 4:5

Uinjilisti unatokana na neon la Kiyunani ikimanisha “kutangaza.”

2 Tim. 4:5, “*Bali wewe uwe na kiasi katika mambo yote, vumulia yote, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza huduma yako.*”

Inamanisha kusema habari njema kuhusu kifo, maziko na kufufuka kwa Yesu.

Uinjilisti ni utendaji kazi wa moyo wa Mkristo.

Ebu tujifunze somo hili zuri leo.

Ni muhimu.

Nafsi ambazo hazisikii na kutii injili hazitaokolewa.

2 Thes. 1:7-9, “*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoangamizwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;*”

Chombo cha nafsi zilizopotea ni mbaya zaidi.

Luka 16:19-31, “*Akasema palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo za zambarau na kitani safi, na kula siku zote kwa anasa. Na maskini mmoja jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kusibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya Yule tajiri; hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake. Ikawa yule maskini alikufa akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa akazikwa. Basi kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali na Lazaro kifuani mwake. Akalia akasema, Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu. Ibrahimu akasema mwanangu kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema yako katika maishaa yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa. Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu. Akasema bassi baba nakuomba, mtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akasema, waanao Musa na manabii; na wawasikilize wao. Akasema, La baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu. Akamwambia wasipowasikiliza Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu.*”

Sehemu ya mateso (maumivu, kilio, na kusaga meno).

Sehemu yenye giza.

Sehemu yenye kumbukumbu.

Ni milele. Mat. 25:46, "*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*"

Kila dakika nafsi zinakufa – je tunazihisi kwa ajili yao? Yesu aliona dharura ya kumwokoa wenye dhambi. Aliwafia.

Paulo alihisi dharura. Kol. 1:28, "*Ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu kwa hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo.*"

Nafsi ambazo hazileti ujumbe zitapotea pia.

Ezek. 3: 16-20, "*Hata ikawa mwisho wa siku saba neon la BWANA likanijia kusema, mwanadamu nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi sikia neon hili litokalo katika kinywa change, ukawape maonyo haya yatokayo kwangu. Nimwambiapo mtu mbaya , hakika utakufa, wewe usimpe maonyo, wala husemi na huyo mtu mbaya ili kumwonya, kusudi aache njia yake mbaya na kujikoa roho yake; mtu yule mbaya atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mikononi mwako. Lakini ukimwonya mtu mbaya, wala yeye hauachi ubaya wake, wala njia yake mbaya atakufa katika uovu wake; bali wewe umejikoa roho yako. Tena mtu mwenye haki aiachapo haki yake, na kutenda uovu name nikiweka kikwazo mbele yake, atakufa; kwa sababu hukumwonya atakufa katika uovu wake, wala matendo yake ya haki aliyoyatenda hayatakumbukwa; lakini damu yake nitaitaka mokononi mwako.*"

Yak. 4:17, "*Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi kwake huyo ni dhambi.*"

Hivyo, uinjilisti unamwokoa mwenye dhambi na mtoa ujumbe.

Unjilisti umeamuriwa

Kusudi la Yesu kuja na kufa ilikuwa ni kumwokoa mwenye dhambi.

1Tim. 1:15, "*Ni neon la kuaminiwa tena lastahili kukubalika ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhaambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.*"

Wote waliokolewa na Mungu wameamriwa kuhubiri na kufundisha.

Marko 16:15-16, "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

Paulo alielewa injili kuwa injili ya upatanishi (wenye dhambi wanapatanishwa na Mungu).

2 Kor. 5: 18-19, "*Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake Kristo, naye alitupa huduma ya upatanishi; yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndaani yetu neno la upatanisho.*"

Mfano: kanisa la kwanza lilichukulia agizo hili kwa umuhimu (Mdo. 8:4).

Uinjilisti unatufanya kuwa watenda kazi wenza wa Mungu.

2 Kor. 6:1, "*Nasi tukitendaa kaazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure.*"

Anatutumia kuitangaza injili yake.

2 Kor. 4:7, "*Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu.*"

Ni heshima kuu kufanya kazi na Mungu katika juhudi hii kuu.

Je unajisikia vizuri ukifanya kazi na Mungu? Je unaifikiria?

Inapaswa kuwa kitu tunachofanya kwa furaha.

Uinjilisti inatenda katika sheria ya kupanda na kuvuna.

Gal. 6:7, "*Msidangaanyike Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.*"

Neno ni mbegu.

Luka 8:11, "*Na huo mfano maana yake ni hii; mbegu ni neno la Mungu.*"

Ni lazima mbegu ipandikizwe kusudi kuwe na mavuno.

Mifano ya Matendo ya Mitume:

Elfu 3000 walizidishwa. Mdo. 2:41, "*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"

Watu elfu 5000. Mdo. 4:4, "*Lakini wengi katika hao waliosikia lile neno waliamini; na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano.*"

Watu wengi. Mdo. 5:14, "*Walioamini wakazidi kuongezeka kwa Bwana, wengi wanaume na wanawake.*"

Tusipofanya uinjilisti (kufundisha neno kwaa waliopotea), wengi watakufa ambao tungesaidia.

Hitimisho

Tunaona umuhimu wa kufanya uinjilisti. Je tunahisi dharura?

Mafanikio yanategemeana na sisi kuweka uinjilisti kuwa nafasi ya juu.